# Dhima za Uradidi katika Mawasiliano ya Kihaya

*Editha Adolph*
*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwl. Nyerere*

**Ikisiri**

**Makala hii inachunguza dhima za uradidi katika mawasiliano ya Kihaya. Eneo ambalo data ya makala hii imepatikana ni kata ya Mayondwe katika wilaya ya Muleba mkoani Kagera. Data ya makala hii imepatikana kwa kutumia mbinu mbili; mbinu ya mahojiano na ya maktabani. Mbinu ya mahojiano imehusisha majibizano baina ya pande mbili, yaani mtafiti na watafitiwa. Lengo la mbinu ya mahojiano ni kupata taarifa zinazohusiana na mada ya makala yetu. Aidha, uteuzi wa mbinu hii ulizingatia ukweli kwamba, mbinu hii husaidia kupata taarifa za ziada ambazo si rahisi kuzipata kwa kutumia mbinu nyingine za ukusanyaji data. Mtafiti aliitumia mbinu ya maktabani kwa kusoma vitabu na makala mbalimbali katika maktaba ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kupata maarifa yanayohusiana na mada ya makala yetu. Halikadhalika, sampuli ya watafitiwa 10 ambao ni wazawa wa mkoa wa Kagera na wazungumzaji wa lugha ya Kihaya ndiyo waliotumika katika makala hii. Vijana walikuwa 5 na watu wazima 5. Data iliyokusanywa imechambuliwa kwa kutumia nadharia ya Uelekeani iliyoasisiwa na McCarthy na Prince (1993, 1994a, 1994b na 1995). Matokeo ya makala hii yanaonesha kuwa uradidi katika lugha ya Kihaya una dhima kadhaa. Mathalani, kufanyika vibaya kwa tendo au ukosefu wa umakini, kufanyika mara kwa mara kwa tendo husika, uharaka wa tendo husika, kudunisha maana, kuongeza msisitizo pamoja na kubadili maana. Inapendekezwa kuwa, tafiti zaidi zifanyike kuhusiana na dhana ya uradidi kwa ujumla. Mathalani, ujitokezaji wa uradidi katika Kihaya kwa kuangazia kategoria za nomino, vielezi, vivumishi, vitenzi nakadhalika. Aidha, utafiti ufanyike kuhusiana na dhima za uradidi katika lugha mbalimbali kama vile: Kiswahili, Kisukuma, Kichaga na lugha nyinginezo.**

**Maneno Muhimu:** Uradidi, Umboghafi, Umbotokeo, Kudunisha Maana, Kuimarisha Maana.

**Utangulizi na Mapitio ya Maandishi**

Dhima za uradidi hujitokeza katika lugha mbalimbali. Aidha, hakuna lugha yoyote duniani yenye dhima moja tu ya uradidi. Dhima za uradidi katika lugha huweza kuwa; kusisitiza jambo, kuonesha hali ya kujirudiarudia kwa hali au tendo fulani, kuonesha wingi na umoja wa dhana husika, uharaka ya jambo, mwendelezo wa hali au tendo fulani, ubora na udhaifu wa dhana fulani, nakadhalika. Ashton (1947) amechunguza matumizi ya uradidi katika lugha ya Kiswahili na kusema kuwa uradidi hutumika kutilia mkazo jambo, kupunguza mkazo wa jambo fulani, kuonesha mueneo wa jambo pamoja na kuonesha mwendelezo wa jambo fulani. Mbali na Ashtoni kuchunguza dhima za uradidi katika Kiswahili, wapo wataalamu mbalimbali (Oden, 1996; Mdee, 1996; Lodhi, 2004) waliochunguza dhima za uradidi. Miongoni mwa dhima hizo ni pamoja na: kurudiarudia kwa tendo, kudhoofisha maana, kuimarisha maana nakadhalika. Kwa mujibu wa Kajitani (2005) ni kwamba, ikiwa uradidi katika lugha yoyote unaweza kudhoofisha maana kwa kupunguza nguvu au sifa za dhana fulani, basi uradidi katika lugha hiyo huweza pia kuwa na dhima ya kuimarisha maana. Naye Tak (2007) amechunguza aina za uradidi katika lugha ya Agta inayozungumzwa nchini Ufilipino pamoja na lugha ya Chichewa inayozungumzwa nchini Malawi. Kutokana na utafiti wake, imegundulika kuwa, maneno mengi katika lugha ya Agta huradidiwa kwa kuhusisha vipandesauti vitatu vya mwanzoni mwa neno husika. Pamoja na maneno mengi kuhusisha uradidi huo, maneno machache ya lugha ya Agta huhusisha uradidi wa vipandesauti viwili. Ili kudhihirisha ukweli huo, Tak anatoa mifano ifuatayo:

| Shina | Maana | Neno Lililoradidiwa | Maana |
|---|---|---|---|
| (a) Ulu | kichwa | ul-ulu | vichwa |
| (b) Takki | mguu | tak-takki | miguu |
| (c) Bari | mwili | bar- bari | miili |
| (d) Wakay | kitu kilichopotea | wak-wakay | vitu vilivyopotea |

**Chanzo:** Tak (2007)

Kutokana na mifano hapo juu, ni dhahiri kuwa viradidiwa vingi katika lugha ya Agta huhusisha uradidi nusu tu na siyo uradidi kamili. Aidha, katika lugha hii, kiradidiwa siyo mfungamano wa vipandesauti isipokuwa ni vipandesauti vya mwanzoni vitatu katika neno husika kama ilivyojitokeza katika (b) – (d). Mbali na viradidiwa vyenye vipandesauti vya mwanzoni vitatu ambavyo ndivyo hujitokeza kwa kiasi kikubwa, vipo viradidiwa vyenye vipandesauti viwili, kwa mfano katika (a) hapo juu ambavyo hujitokeza kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na vile vyenye vipandesauti vitatu.

Halikadhalika, katika utafiti wake, Tak amegundua kuwa lugha ya Chichewa ni lugha yenye uradidi kamili tu ambapo shina ndilo huradidiwa kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

| Shina | Maana | Neno Lililoradidiwa | Maana |
|---|---|---|---|
| (a) gulidwa | nunuliwa | gulidwa + gulidwa | nunuliwanunuliwa |
| yaɳana | angalia | yaɳana + yaɳana | angaliaangalia |
| (b) lemba | andika | lemba + lemba | andikaandika |
| gula | nunua | gula + gula | nunuanunua |
| (c) mwa | kunywa | imwa + imwa | kunywakunywa |
| dya | kula | idya+idya | kulakula |

**Chanzo:** Tak (2007)

Mifano iliyooneshwa hapo juu inahusisha uradidi wa vitenzi vyenye silabi tatu, mbili na hata silabi moja. Mfano katika (a) unaonesha uradidi wa vitenzi vyevye silabi tatu. Uradidi katika vitenzi hivi huhusisha shina zima la kitenzi husika. Vitenzi katika (b) ni vile vyenye silabi mbili. Vitenzi vya aina hii katika lugha ya Chichewa huhusisha uradidi wa shina zima. Aidha, mifano katika (c) imehusisha vitenzi vyenye silabi moja. Kwa mujibu wa Tak (2007), vitenzi vyenye silabi moja katika lugha ya Chichewa haviradidiwi vikiwa pekee isipokuwa huhusisha uchopekaji wa irabu /i/. Ili uradidi ufanyike katika vitenzi hivi, lazima kwanza ufanyike mchakato huo wa uchopekaji wa irabu /i/. Baada ya uchopekaji huo kufanyika, ndipo vitenzi hivyo huweza kuradidiwa kama ilivyojidhihirisha katika (c) hapo juu.

Tofauti na wataalamu waliochunguza mazingira ya ujitokezaji wa uradidi katika lugha mbalimbali, wapo wataalamu waliochunguza dhima za uradidi katika lugha kadha wa kadha. Mathalani, Mwita (2008) ameshughulikia dhima za uradidi katika lugha ya Kuria. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa urudiaji wa tendo katika lugha ya Kuria huonesha msisitizo au mwendelezo wa tukio au tendo husika. Utafiti huu unaonesha pia kuwa uradidi huweza kusababisha kitenzi kimoja kubeba maana zaidi ya moja kwa wakati mmoja. Anaendelea kueleza kuwa uradidi katika lugha hiyo huonesha kufanyika bila umakini kwa tendo au tukio fulani. Mwita anaongeza kwa kusema kuwa uradidi husababisha tofauti za kimaana katika vitenzi. Tofauti na wataalamu hawa; (Kajitani, 2005; Tak 2007; Mwita 2008) waliochunguza dhana ya uradidi katika lugha mbalimbali mathalani, lugha ya Chichewa na Kuria, wapo pia wataalamu walioshughulikia dhima za uradidi katika lugha ya Kiswahili. Mathalan, Mnenuka (2010) ameshughulikia dhima za uradidi katika lugha ya Kiswahili kwa kuangazia kategoria za kileksika. Miongoni mwa kategoria alizoshughulikia mtaalamu huyu ni pamoja na: nomino, vivumishi, vitenzi na vielezi. Katika utafiti wake amebainisha kuwa uradidi una dhima ya kuimarisha na kudhoofisha maana. Anatoa mifano ifuatayo inayoonesha uimarishaji na udhoofishaji wa maana unaotokana na uradidi katika nomino za Kiswahili:

| A | B |
|---|---|
| Basi lilisimama maeneo ya Mikumi-Mikumi. | Basi lilisimama Mikumi. |
| Baraka anatokea maeneo ya Mtwara-Mtwara. | Baraka anatokea Mtwara. |
| Tulimuona Neema maeneo ya Chalinze-Chalinze. | Tulimuona Neema Chalinze. |

**Chanzo**: Mnenuka (2010)

Mifano iliyotolewa katika safu A inaonesha kutokuwa na uhakika wa kile anachozungumza mzungumzaji. Mifano iliyotolewa katika safu B ni tofauti na ile ya safu A kwani mzungumzaji ana hakika na kile anachokizungumza. Kutokana na mifano hii, Mnenuka (2010) anasema kuwa mifano ya safu B inaonesha kuwa mzungumzaji ana hakika na kile anachokisema; kama anachokisema ni kweli au si kweli, hilo linabaki kwa mzungumzaji mwenyewe. Mtaalamu huyu anaendelea kutoa mifano ifuatayo ili kuonesha ni kwa jinsi gani uradidi huweza kuimarisha na kudhoofisha maana katika lugha ya Kiswahili:

| A | B |
|---|---|
| Mtu wa chini. | Mtu wa chini-chini. |
| Chibichi alicheza mpira pembeni. | Chibichi alicheza mpira pembeni-pembeni. |

**Chanzo**: Mnenuka (2010)

Mnenuka (keshatajwa), anadhihirisha wazi kuwa uradidi uliojitokeza katika vielezi vya mahali kama vile *chini-chini* na *pembeni-pembeni* umesababisha kudhoofika kwa maana ikilinganishwa na vile ambavyo havikufanyiwa uradidi. Anafafanua kuwa kielezi *chini* humaanisha chini kabisa ilhali kielezi *chini-chini* humaanisha chini kiasi vivyo hivyo na katika kielezi *pembeni* na *pembeni-pembeni*. Mbali na wataalamu hawa, wapo pia walioshughulikia dhana ya uradidi kwa ujumla. Miongoni mwao ni: Wataalamu tuliowapitia wameshughulikia uradidi katika Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu kama vile Chichewa na Kuria. Tofauti na makala hii, hakuna utafiti uliochunguza dhima za uradidi katika mawasiliano ya lugha ya Kihaya. Makala ya sasa inashughulikia eneo hilo.

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uelekeani. Nadharia hii iliasisiwa na McCarthy na Prince (1993, 1994a, 1994b na 1995). Uelekeani ni uhusiano wa vipengele viwili ambavyo ni shina na kiradidiwa. Msisitizo wa nadharia hii ni kwamba, lazima uadilifu utumike katika kufanya mchakato wa uradidi kati ya umboghafi na umbotokeo kwa mujibu wa kanuni, sheria na taratibu za lugha husika. Endapo umboghafi na umbotokeo (umboradidiwa) havitakuwa na uelekeani basi hilo umbo litakuwa limekiuka kanuni, sheria na taratibu za lugha husika na hivyo umbo hilo litakuwa halina maana sahihi katika lugha husika.

McCarthy na Prince (1993, 1994a, 1994b na 1995) wanasema kuwa ni muhimu utambulisho wa kiini na kiradidiwa uendane na lugha husika. Aidha, kila lugha ina utaratibu wake unaojitosheleza katika suala zima la uundaji wa maneno kutokana na mchakato wa uradidi. Hii ni kwa sababu kila lugha ina utaratibu wake unaojitosheleza katika suala zima la uundaji wa maneno kutokana na mbinu ya uradidi. Waasisi hawa wanaendelea kusisitiza kuwa kila lugha ina utaratibu wake unaofuatwa katika kupangilia kiradidiwa. Kutokana na utaratibu huu kiradidiwa kinaweza kujitokeza kabla au baada ya mzizi au shina la neno.

Aidha, nadharia hii inadai kuwa suala la ukubalifu kwa maana ya usahihi wa maana ya maneno yaliyoradidiwa katika lugha yoyote ile, lazima uzingatiwe katika uradidi kwani ukubalifu huo unadhibiti uundaji wa maneno radidi yasiyokubalika katika lugha husika. Ukubalifu unaoongelewa hapa ni ule unaoshughulikia vipengele vya ziada vinavyoweza kuvunja uelekeani uliopo baina ya kiinineno na kiradidiwa. Aidha, ukubalifu huu ni ule unaohakikisha kuwa umbo unde halikiuki taratibu za lugha husika. Kama ambavyo nadharia hii iliwaongoza waasisi wake kwa kutoa mwongozo ni kwa namna gani ya kuweka uelekeani kati ya umboghafi na umbotokeo katika lugha walizofanyia utafiti, hivyohivyo nadharia hii imemwongoza mtafiti wa sasa. Mtafiti wa makala hii ameweza kupata mwongozo ni kwa jinsi gani anaweza kupata maumbo kubalifu baada ya umboghafi kufanyiwa uradidi hadi kufikia hatua ya kuwa umbotokeo. Kwa kufanya hivyo, maneno yaliyoradidiwa yameweza kuwa na uelekeani na maneno yasiyoradidiwa. Kutokana na hali hii ndipo sasa tumeweza kupata dhima za maumbotokeo yaliyofanyiwa uradidi.

**Mbinu za Utafiti**

Katika utafiti huu, wametumia mbinu mbalimbali za kiutafiti ili kufikia malengo yao. Mbinu za ukusanyaji data ni mbinu zinazochaguliwa na mtafiti kwa lengo la kukusanya data ya utafiti wake (Kothari, 2004). Kwa mujibu wa Kitchin na Tate (2000) kuchagua njia ya kukusanyia data si kuchagua njia yoyote inayoonekana rahisi kuitumia, bali ni kuchagua njia inayojitosheleza na inayohusiana na kile unachokitafiti. Utafiti huu umefanyika katika Mkoa wa Kagera, Wilayani Muleba katika kata ya Izigo. Mtafiti ameteua eneo hilo kutokana na kuwapo kwa vyanzo vya data inayohitajika kwa ajili ya makala hii. Aidha, ndiko wazungumzaji wa lugha ya Kihaya ambayo ndiyo inayotafitiwa inakozungumzwa. Maeneo haya yameteuliwa pia kutokana na sababu kuwa ni vigumu kwa mtafiti kukusanya data kutoka katika maeneo mengi yenye wazungumzaji wa Kihaya kutokana na ufinyu wa bajeti na muda uliopangwa kwa ajili ya utafiti huu. Maeneo yaliyoteuliwa yamewezesha upatikanaji wa data ya kutosha iliyotumika katika makala yetu.

Mtafiti ametumia njia ya hojaji na chanzo cha data cha maktabani katika zoezi la kukusanya data ya makala hii. Hojaji ni orodha ya maswali na maelekezo yaliyoandaliwa na mtafiti ili yaweze kujibiwa na watafitiwa kwa lengo la kukusanya data ya utafiti. Njia ya hojaji iliteuliwa katika makala hii kwani njia hii humpa mtafitiwa uhuru wa kutoa majibu bila woga. Pia hojaji huweka ulinganifu wa majibu yanayotolewa na watafitiwa wote. Kutokana na njia hii, wazungumzaji wa Kihaya 20, (vijana 10, wa kike 5 na wa kiume 5, watu wazima 10, wanawake 5 na wanaume 5) walijaza hojaji ambapo mtafiti alihitaji orodha ya maneno yenye uradidi katika lugha ya Kihaya. Aidha, uteuzi wa idadi hii ya watafitiwa ulijumuisha wazungumzaji wa lahaja ya Kihamba ambayo ni lahaja mojawapo ya lugha ya Kihaya na ndiyo inayoshughulikiwa katika makala hii. Chanzo cha data cha maktabani kilijumuisha usomaji wa nyaraka za kitaaluma kwa lengo la kupata data muafaka. Nyaraka zilizosomwa ni tasnifu mbalimbali, vitabu vinavyohusu uradidi unavyofanyika katika lugha mbalimbali na nyaraka mbalimbali za kitaaluma. Aidha, data iliyokusanywa ilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli (usio wa kiidadi). Mkabala huu umetoa mwanya wa kuchanganua data kwa kutoa maelezo pasipo kubanwa na taratibu za kitakwimu. Makala hii yanachunguza dhima za uradidi katika Kihaya. Tuangalie dhima hizo katika kipengele kinachofuatia hapa chini.

**Dhima za Uradidi katika Lugha ya Kihaya**

Uradidi ni dhana inayojitokeza katika lugha mbalimbali kwa lengo la uboreshaji wa msamiati uliopo ili uweze kubeba dhana za ziada. Dhima za radidi katika lugha, tukiachilia mbali dhima nyingi nyingine, uradidi unaweza kuwa na dhima kama vile: kuonesha uharaka wa jambo au tukio fulani, kuonesha kufanyika mara kwa mara kwa tendo husika, kuonesha wingi, kuongeza msisitizo, kubadili maana ya neno, kuongeza msamiati katika lugha, kuonesha kufanyika vibaya kwa jambo au ukosefu wa umakini katika tendo husika pamoja na kudunisha maana. Kwa mujibu wa Novotna (2000) Uradidi katika lugha huonesha kuendelea na kurudiwa kwa jambo fulani, huongeza msamiati katika lugha, huamisha maana, hushadidia jambo na kubadili maana.

**Kufanyika kwa Jambo Pasipo Mpangilio Maalumu au Ukosefu wa Umakini**

Uradidi huweza kuonesha ni kwa jinsi gani tendo fulani linavyoweza kutendwa bila umakini au kufanyika bila mpangilio maalumu. Katika kipengele hiki, umboghafi (neno la kwanza lisiloradidiwa) huweza kuonesha umakini wakati wa kutenda jambo fulani lakini umbotokeo (neno radidiwa) linalotokana na umboghafi (lisiloradidiwa), huweza kuonesha ni kwa jinsi gani tendo husika limefanywa vibaya au bila umakini hata bila kuwa na mpangilio maalumu. Tuangalie mifano ifuatayo ili kuelewa zaidi dhana hii:

**Kielezo: 1. Kufanyika kwa Jambo Pasipo Mpangilio Maalumu au Ukosefu wa Umakini**

| | |
|---|---|
| chwa | chwachwa/chweleleza |
| gamba | gambagamba |
| nyamula | nyamunyamula nyamanyamula |
| shwela | shweleleza |
| zala | zalazala/zaliliza |

Mifano hapo juu inaonesha kufanyika kwa jambo pasipokuwa na umakini au kufanya jambo vibaya au hovyohovyo. Aidha, inadhihirisha wazi kuwa mtenda wa tendo husika hana mpangilio maalumu kwa tendo hilo. Neno la Kihaya *chwa* humaanisha *tema* katika Kiswahili. Neno hili baada ya kufanyiwa mchakato wa uradidi yakapatikana maneno ya Kihaya *chwachwa* au *chweleleza* ambayo yanamaanisha kutema hovyohovyo. Yumkini yaweza kuwa kutema mate, chakula au maji, kutoka katika kinywa ama cha binadamu, mnyama au mdudu nakadhalika. Umboghafi yani neno la kwanza ambalo halijafanyiwa uradidi; neno *chwa*, linaonesha umakini kutokana na tendo husika. Lakini umbotokeo ambalo ni neno *chwachwa* au *chweleleza* maana yake tendo hilo limefanyika bila umakini au limefanyika hovyohovyo. Neno la Kihaya *gamba*, humaanisha *ongea* katika Kiswahili. Neno hili baada ya kuradidiwa tunapata neno *gambagamba* ambalo linarejelea tendo la kuongea hovyohovyo pasipokuwa na umakini katika kile kinachoongelewa ama kuongelea suala fulani bila mpangilio maalumu.

Data ya makala hii inaonesha kuwa neno la Kihaya *nyamula* pia lina uwezo wa kufanyiwa uradidi. Maana ya neno *nyamula* ni chana. Mathalani, kuchana nguo, karatasi, nakadhalika. Baada ya neno hili kuradidiwa tumepata neno *nyamulanyamula* ambalo humaanisha tendo la kuchanachana bila mpangilio au kufanya tendo hilo hovyohovyo. Aidha, neno la Kihaya *shwela* ni tendo la kuoa. Neno hili likiradidiwa katika Kihaya tunapata neno *shweleleza* ambalo linamaanisha tendo la kuoa hovyohovyo ama kuoa pasipokuwa na mpangilio maalumu. Hivyo, mwanaume husika anakuwa na tabia ya kuao wanawake wengi na hatulii na mwanamke mmoja. Yawezekana akaoa wanawake zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja au anaoa na kufukuza. Matokeo ya makala yetu yanaonesha pia kuwa uradidi huweza kufanyika katika neno *zala*[1] la Kihaya linalorejelea dhana ya kuzaa. Neno hili hujitokeza kama *zalazala* baada ya kufanyiwa mchakato wa uradidi. Neno hili (*zalazala*) linarejelea tendo la kuzaa bila mpangilio au kuzaa hovyohovyo. Baada ya kuangalia dhima ya uradidi ya kufanyika vibaya kwa tendo au ukosefu wa umakini tuone dhima nyinginezo za uradidi katika lugha ya Kihaya.

**Kufanyika Mara kwa Mara kwa Tendo Husika**

Dhima nyingine ya uradidi katika lugha ya Kihaya ni kuonesha kutendeka mara kwa mara kwa tendo husika. Yapo maneno kadhaa ambayo yakitamkwa pasipo kuradidiwa hurejelea dhana ya kufanyika mara moja kwa tendo husika au kutokuwa bayana kama tendo hilo limefanyika mara moja au hufanyika mara kwa mara. Lakini pale maneno hayo yanapofanyiwa uradidi, moja kwa moja hurejelea dhana ya kufanyika mara kwa mara kwa tendo husika. Aidha, mara nyingi maneno yanayoonesha kufanyika vibaya au hovyohovyo kwa tendo fulani, pia maneno hayo hayo huonesha

[1] Zala katika Kihaya hurejelea tendo la kuleta kiumbe kipya duniani. Hutumika kwa binadamu, wanyama, wadudu, mimea nakadhalika. Suala hili ni tofauti katika lugha ya Kiswahili ambapo neno kujifungua hutumika kwa binadamu na kuzaa hutumika kwa viumbe vinginevyo kama wanyama, wadudu, mimea nakadhalika.

kufanyika mara kwa mara kwa tendo husika. Tuangalie mifano ifuatayo ili kuelewa dhana hii kwa urahisi zaidi.

**Kielezo: 2. Kufanyika Mara kwa Mara kwa Tendo Husika**

| | |
|---|---|
| lwala | lwalalwala |
| shaba | shabashaba |
| tela | telatela/teleleza |
| tonga | tongatonga |
| yosha | yoshayosha |

Katika mifano yetu tuna neno la Kihaya *lwala* lenye maana ya kuugua. Data ya makala yetu inaonesha kuwa neno hili hukubali mchakato wa uradidi. Baada ya kufanyiwa uradidi, neno hili limejitokeza kama *lwalalwala* lenye kumaanisha ugua mara kwa mara. Nalo neno la Kihaya *shaba* maana yake ni omba. Baada ya kufanyiwa uradidi neno hili limejitokeza kama *shabashaba* lenye kumaanisha tendo la kuomba mara kwa mara. Matokeo ya makala yetu yanaonesha pia kuwa neno la Kihaya *tela* huweza kufanyiwa uradidi. Maana ya neno hili katika Kiswahili ni piga. Baada ya neno hili kufanyiwa uradidi limejitokeza kama *telatela* au *teleleza*. Katika Kihaya neno *tonga* pia hukubali mchakato wa uradidi. Katika Kiswahili neno hili humaanisha kudai. Baada ya kufanyiwa mchakato wa uradidi neno hili hujitokeza kama *tongatonga.* Mzungumzaji wa Kihaya akisema; *nanka atongatonga* au *ensi nanka etongatonga*, maana yake ni kuwa; mtu fulani au taifa fulani hudai mara kwa mara au mara nyingi. Halikadhalika, matokeo ya makala yetu yanathibitisha kuwa miongoni mwa maneno ya Kihaya yanayokubali kupokea mchakato wa uradidi ni neno *yosha*. Neno *yosha* linarejelea tendo la mtu kutokuwa mahala anakotakiwa kuwa. Yaweza kuwa mwanafunzi kutohudhuria shuleni, mfanyakazi kutokuwa katika kituo chake cha kazi bila kutoa taarifa nakadhalika. Dhana tunayoipata kutokana na neno *yosha* ni kwamba tendo hilo limefanyika mara moja. Lakini, neno hilohilo baada ya kuradidiwa na kuwa *yoshayosha* tayari inarejelea tendo la mtu kutokuwa katika eneo husika mara kwa mara pasipo kutoa taarifa kwa wahusika.

**Uharaka wa Tendo Husika**

Data ya makala hii inaonesha pia kuwa moja ya dhima za uradidi katika lugha ya Kihaya ni kuonesha uharaka wa tendo husika. Imethibitika kuwa baadhi ya maumbotokeo (maneno yaliyoradidiwa) ya Kihaya huonesha hali ya tendo kufanyika haraka zaidi kuliko umboghafi (maneno yasiyoradidiwa). Mifano ifuatayo inaweka bayana ukweli huo:

**Kielezo: 3. Uharaka wa Tendo Husika**

| **A** | **B** |
|---|---|
| byala | byalabyala |
| chumba | chumbachumba |
| lima | limalima |
| tambuka | tambukatambuka |
| yoga | yogayoga |

Mifano hapo juu inathibitisha kuwa baadhi ya maneno ya Kihaya yakifanyiwa uradidi mathalani, maneno katika safu A yanaonesha uharaka wa tendo husika tofauti na yale ya safu B. Kwa mfano, maneno yote ya safu A yanaonesha kufanyika kwa tendo katika hali ya kawaida. Wazungumzaji wa Kihaya wanapohitaji kumtaka mtu afanye tendo husika kwa haraka basi hutumia maneno ya safu B kama yalivyobainishwa hapo juu. Kutokana na mifano yetu, neno la Kihaya *byala* humaanisha panda au siha. Dhana ya kupanda inayoongelewa hapa ni ile ya kuweka mazao ardhini au kusiha mbegu. Pale linapofanyiwa uradidi neno hili, hujitokeza kama *byalabyala* na hurejelea tendo la kupanda au kusiha harakaharaka. Aidha, neno *chumba* la Kihaya, maana yake ni pika. Pale neno hili linapofanyiwa uradidi na kuwa *chumbachumba* linamaanisha pika harakaharaka. Neno jingine kwa mujibu wa data yetu ni *lima*. Maana ya neno hili hubaki ileile katika lugha zote mbili yaani Kihaya na Kiswahili ambalo humaanisha uzalishaji wa mazao mbalimbali. Mazao hayo yaweza kuwa ya chakula au biashara. Baada ya neno hili kuradidiwa na kuwa *limalima*, hurejelea dhana huyohiyo ya kulima isipokuwa katika hali ya uharakaharaka. Halikadhalika, neno la Kihaya *tambuka* lenye kumaanisha tembea, likiradidiwa tunapata neno *tambukatambuka* lenye kumaanisha tembea harakaharaka. Aidha, matokeo ya makala yetu yanaonesha kuwa neno *yoga* lina uwezo wa kuradidiwa. Maana ya neno hili ni oga. Neno hili likifanyiwa uradidi linakuwa *yogayoga* na neno hili linarejelea dhana ya kufanya tendo la kuoga harakaharaka.

**Kudunisha Maana**

Miongoni mwa dhima za uradidi katika lugha ya Kihaya ni kudunisha maana. Hii ni kwa mujibu wa data ya makala hii. Yapo baadhi ya maneno ambayo yakitamkwa au kuandikwa pasi na kuradidiwa basi maneno hayo huwa na uzito kwa kile kinachoongelewa au kuimarisha maana ya dhana husika. Pale tu maneno hayo yanaporadidiwa moja kwa moja hudunisha maana hiyo. Dhima hii hujitokeza kwa baadhi ya maneno ya Kihaya kama inavyoonekana katika mifano hapa chini:

**Kielezo: 4. Kudunisha Maana**

| A | B |
|---|---|
| enjala | enjalajala |
| lemwa | lemwalemwa |
| murungi | murungirungi |
| obushuma | obunshumanshuma/orunshumanshuma |
| yokya | yokyayokya |

Kutokana na data yetu hapo juu imethibitika kuwa maneno yote yaliyo katika safu A yanarejelea ubora wa dhana husika, uimara wake, ukubwa, wingi, upana wa dhana hiyo, tofauti na maneno yaliyo katika safu B ambayo yanadunisha dhana hizo. Mathalani, neno la Kihaya *enjala* maana yake ni njaa. Neno hili likifanyiwa uradidi tunapata neno jipya la Kihaya, *njalajala*. Kwa mfano, mzungumzaji wa Kihaya akisema, '*nimpulila enjala*' (nahisi njaa) maana yake ni kuwa mtu huyo anahisi kiasi kikubwa cha njaa. Lakini akihitaji kuonesha ni kwa namna gani anahisi kiasi kidogo cha njaa basi atasema, '*nimpulila orujalajala au enjalajala*' (nahisi njaanjaa). Katika safu A pia tunaona neno la Kihaya *lemwa*. Maana ya neno hili ni choka. Neno hili limejitokeza kama *lemwalemwa* katika safu B baada ya kupitia mchakato wa uradidi. Neno radidiwa (*lemwalemwa*) limedunisha maana ya neno la mwanzo kwani neno la mwanzo linarejelea uchovu hasa, tofauti na neno la pili (neno radidiwa) ambalo linarejelea uchovu wa kiwango cha chini.

Matokeo ya makala yetu yanathibitisha pia kuwa neno la Kihaya *murungi* lenye maana ya mzuri, nalo hukubali mchakato wa uradidi. Dhana tunayoipata kutokana na neno murungi[2] ni kwamba mtu husika anakuwa na uzuri wa kiwango cha juu. Tofauti na maana hiyo, tunapoliradidi neno hili na kuwa *murungirungi* basi maana tunayoipata ni tofauti na maana ya mwanzo. Neno radidiwa *murungirungi* linarejelea uzuri wa kiwango cha chini ikilinganishwa na neno *murungi* kama ilivyodadavuliwa hapo juu. Data ya makala hii inadhihirisha pia kuwa neno la Kihaya *obushuma* hufanyiwa mchakato wa uradidi. Maana ya *obushuma* ni wizi. Baada ya kuradidiwa kwa neno hili tunapata neno *obunshumanshuma* au *orunshumanshuma*. Maana ya neno *obunshumanshuma* au *orunshumanshuma* ni hali ya kuwa na wiziwizi. Hivyo, ni Dhahiri kuwa neno radidiwa linadunisha hali hiyo ya wizi kutoka katika kiwango cha juu na kuwa katika kiwango cha chini. Kwa hiyo wazungumzaji wa Kihaya wakisema *nanka mshuma*, (fulani ni mwizi) maana yake mtu huyo amekubuu katika tabia ya wizi. Isipokuwa wakisema *nanka aina obunshumanshuma* (fulani ni mwizimwizi) maana yake mtu huyo ni mdokozi wa vitu vidogovidogo. Aidha, neno la Kihaya *yokya* humaanisha choma. Neno hili hurejelea dhana ya kuchoma kikamilifu. Yaweza kuwa uchomaji wa nyama, nguo, nyumba na vitu vingine vinavyoweza kuchomeka kwa moto. Neno radidiwa *yokyayokya* lenye kumaanisha chomachoma huidunisha dhana hiyo na kumaanisha kuchoma kwa kiwango cha chini. Ina maana vitu vilivyotajwa hapo juu vitachomwa kidogo au kwa juujuu. Mbali na maana hiyo, neno *yokya* pia humaanisha hali ya mwili kuwa na joto. Hivyo, neno *yokya* katika muktadha huu, linarejelea mwili kuwa na joto la juu mathalani $39^\circ/40^\circ$ ilhali neno *yokyayokya* likirejelea joto la kiwango cha kati kwa mfano $37.5^\circ/38^\circ$ isipokuwa si la kawaida yaani si $36.5^\circ/37^\circ$. Mbali na dhima ya uradidi ya kudunisha maana, tuangalie dhima nyingine ambayo ni kuongeza msisitizo.

**Kuongeza Msisitizo**

Mbali na dhima mbalimbali za uradidi katika Kihaya zilizobainishwa hapo juu, imebainika pia kuwa uradidi hufanya kazi ya kusisitiza jambo fulani. Rubanza (1996) anafafanua kuwa uradidi unaweza kutumika katika, mosi: kuimarisha au kudhoofisha maana. Pili: kupunguza au kuongeza msisitizo wa dhana inayozungumziwa. Mtazamo huu una ukweli kwani ni dhahiri kuwa dhima hizi pia zinajitokeza katika lugha ya Kihaya kutokana na mchakato wa uradidi. Ifuatayo ni mifano inayoonesha ni kwa jinsi gani uradidi huongeza msisitizo katika lugha ya Kihaya:

**Kielezo: 5. Kuongeza Msisitizo**

| SAFU A | SAFU B |
|---|---|
| ge | geigeige |
| muno | munomunonga |
| mwaha | mwahamwaha |
| mwana wange | mwana wangenyabwange |
| mwendo guya | mwendo guyaya |
| yagwa kwo | yagwa kwokwokwo |

[2] Uzuri unaorejelewa hapa ni wa sura, umbo na matendo mema.

Katika Kielelezo 5 hapo juu tunaona kuwa maneno yaliyo katika safu A hayajafanyiwa uradidi na yaliyo katika safu B yamefanyiwa mchakato wa uradidi. Maneno ya safu B yanaweka msisitizo zaidi juu ya dhana inayopatikana katika maneno ya safu A. Kwa hiyo, maneno ya safu A hayana msisitizo juu ya dhana zinazotokana nayo na kama utakuwepo basi ni kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na yale ya Safu B. Mathalani, maana ya kivumishi *ge* ni vizuri au vema. Kivumishi hiki kinaporadidiwa na kuwa *geigeige*, basi husisitiza na kuonesha kuwa tendo husika limefanyika vizuri au vema sana. Kielezi *muno* humaanisha sana. Kielezi hiki kikifanyiwa mchakato wa uradidi, tunapata kielezi *munomunonga*. Kielezi kilichopatikana baada ya kuradidiwa kinaweka msisitizo mkubwa juu ya jambo husika kwamba liko katika hali ama mbaya sana au nzuri sana. Kwa mfano, tukisemea juu ya shule; kama tunaongelea uzuri wa shule (yaweza kuwa mazingira au ufaulu); '*shule ndungi munomunonga*' basi itakuwa katika hali nzuri sana. Na kama ni kwa upande wa ubaya; '*shule mbi munomunonga*,' basi shule hiyo itakuwa na hali mbaya sana ama katika kufaulisha au kimazingira. Aidha, kielezi *mwaha* humaanisha sasa hivi. Wazungumzaji wa Kihaya wanaposema *mwahamwaha* humaanisha muda huhuhuu. Hivyo, kielezi hiki *mwahamwaha* maana yake kama kuna tendo inabidi lifanyike basi lazima lifanyike ndani ya muda huohuo bila kupoteza hata dakika moja. Kirai *mwana wange*, humaanisha mtoto wangu. Kirai hiki kinaweza kuwa kinamaanisha kuwa mtoto anayeongelewa ni wa msemaji kabisakabisa kwa maana ya kumzaa ama ni wa ndugu yake lakini pia anaweza kuwa tu mlezi. Pale kirai hiki kinaporadidiwa na kuwa mwana *wangenyabwange* huweka msisitizo kuwa mtoto anayeongelewa ni wa msemaji fika. Yani ni mtoto wake wa kumzaa. Matokeo ya makala hii yanaonesha pia kuwa kielezi cha Kihaya *kwo* hukubali mchakato wa uradidi. Kabla ya kuradidiwa, kielezi hiki humaanisha hasa. Baada ya kufanyiwa mchakato wa uradidi na kuwa *kwokwokwo*, maana yake inakuwa hasahasa au kwelikweli. Kwa hiyo kirai *yagwa kwo* maana yake ni kitu fulani, chaweza kuwa mvua, gari, mtu au kifaa chochote kile kwamba kimeanguka kweli. Kama ni mvua imenyesha kweli. Lakini kirai *yagwa kwokwokwo* maana yake ni kuwa kitu hicho kimeanguka haswa. Kama ni gari basi tunaweza kusema limeanguka na kuwa nyang'anyang'a. Kama ni mvua imenyesha haswa. Baada ya kuona dhima ya msisitizo itokanayo na mchakato wa uradidi, tuangalie dhima nyingine ya uradidi katika Kihaya ambayo ni kubadili maana husika.

**Kubadili Maana**

Mbali na dhima mbalimbali za uradidi zilizofafanuliwa hapo juu, pia uradidi katika lugha ya Kihaya hubadili maana ya mwanzo. Kwa hakika, neno radidiwa hutokana na neno la mwanzo lisiloradidiwa. Baada ya neno la mwanzo kupitia mchakato wa uradidi, huweza kuwa na dhima kadhaa hususan kubadili maana. Tuangalie mifano hapa chini kwa uelewa zaidi.

**Kielezo: 6. Kubadili Maana:**

| SAFU A | SAFU B |
|---|---|
| amagezi | amagezigezi |
| bashatu | bashatubashatu |
| humula | humulahumula |
| kyona | kyonakyona |
| ngemu | ngemugemu |

Mifano katika kielelezo chetu hapo juu inaonesha jinsi maana ya maneno ya safu A inavyotofautiana na maana ya maneno ya safu B ingawa maneno ya safu B yametokana na yale ya safu A. Mathalani, neno *amagezi* humaanisha akili katika lugha ya Kiswahili. Baada ya neno hili

kufanyiwa uradidi tumepata neno *amagezigezi* ambapo maana imebadilika na kuwa hali ya mtu kuwa mdanganyifu. Aidha, neno *bashatu* hurejelea watu watatu katika lugha ya Kiswahili. Neno radidiwa *bashatubashatu* halirejelei maana hiyo tena isipokuwa hurejelea zaidi ya watu watatu. Aidha, watu hawa wanakuwa katika makundi ya watu watatuwatatu. Aidha, neno *humula* humaanisha Upande wa safu A pia kuna neno *kyona* ambalo hurejelea kitu kizima au chote. Kwa maana kuwa kama ni kitu fulani basi kiwe kizima. Lakini neno hili likifanyiwa mchakato wa uradidi na kuwa *kyonakyona* maana yake hubadilika na kuwa chochote kile (kitu chochote kile). Halikadhalika, neno la Kihaya *ngemu* lililo katika safu A hurejelea aina zote za migomba. Baada ya kufanyiwa mchakato wa uradidi neno hili limekjitokeza kama *ngemugemu*. Maana ya neno radidiwa imebadilika na kuwa aina moja tu ya mgomba. Aina hii ya mgomba ni tofauti na aina zote za migomba kwani ndiyo husitawisha ndizi ziliwazo na Wahaya ambazo hujulikana kama ndizi Bukoba.

**Kuhimiza Jambo**

Kwa mujibu wa matokeo ya makala yetu ni kwamba, uradidi katika lugha ya Kihaya huonesha uhimizaji wa jambo fulani. Kwa kutamka neno bila kulirudiarudia humaanisha kuwa msemaji hajaweka msisitizo katika kile kinachosemwa. Msemaji huonesha kusisitiza jambo pale anapoongea kwa kulirudiarudia. Mifano ifuatayo inathibitisha zaidi.

**Kielezo: 7. Kuhimiza Jambo:**

| SAFU A | SAFU B |
|---|---|
| ganyila | ganyilaganyila |
| humula | humulahumula |
| ija | ijaijaija |
| lekela | lekelalekelalekela |
| shoma | shomashomashoma |

Kutokana na mifano iliyotolewa katika kielelezo 7 hapo juu, ni dhihiri kuwa uradidi huonesha hali ya kusisistiza jambo fulani. Mzungumzaji wa Kihaya akisema au mwandishi akiandika neno *ganyila* anamaanisha hurumia au samehe. Endapo atarudiarudia neno hili kwa kuandika au kusema; *ganyilaganyila* maana yake anamsisitiza mhusika asamehe kabisa. Kwa maana nyingine msemaji asiporudiarudia neno hilo maana yake hakuna umuhimu sana wa mhusika kusamehewa, lakini pale anapotamka ama kuandika kwa kulirudiarudia maana yake anamsisitiza aliyekosewa atoe msamaha au awe na huruma kwa kile alichokosewa. Aidha, neno *humula* hurejelea tendo la kumnyamazisha mwenye uchungu. Maana ya pili ya neno hili ni pumzika. Endapo neno hili litatumika bila kuradidiwa, basi neno linakuwa halioneshi msisitizo wowote. Pale linapotumika kwa kurudiwarudiwa kama *humulahumula* huonesha msisitizo wa kumnyamazisha mhusika au kumtaka apumzike. Tofauti na neno hilo, kuna neno jingine ambalo ni *ija*. Maana ya neno ija ni *njoo*. Neno hili linapotumika bila kuradidiwa, maana yake ni kwamba hakuna msisitizo juu yake. Pale neno *ija* linaporadidiwa mara mbili tu na kuwa *ijaija* msisitizo wake unakuwa mdogo ikilinganishwa na pale linaporadidiwa mara tatu ijaijaija. Aidha neno la Kihaya *lekela* hurejelea hali ya kuacha jambo fulani. Endapo neno hili likiradidiwa mara mbili na kuwa *lekelalekela* msisitizo wake utakuwa mdogo ikilinganishwa na neno ambalo limeradidiwa zaidi ya mara mbili na kuwa *lekelalekelalekela*. Nalo neno *shoma* maana yake ni soma. Endapo neno hili litaradidiwa tukapata neno *shomashomashoma* basi neno hili litakuwa linaonesha msisitizo wa hali ya juu. Aidha, neno hili huweza kuradidiwa mara nyingi kulingana na

msisistizo unaotakiwa kuoneshwa pia kadri linavyozidi kurudiwarudiwa ndivyo na toni yake hubadilika.

**Hitimisho**

Makala hii imechunguza dhima za uradidi katika mawasiliano ya Kihaya. Matokeo yanaonesha kuwa uradidi una dhima mbalimbali katika lugha ya Kihaya. Miongoni mwa dhima hizo ni pamoja na kufanyika kwa jambo pasipo mpangilio maalumu au ukosefu wa umakini, kufanyika mara kwa mara kwa tendo husika, uharaka wa tendo husika, kudunisha maana, kuongeza msisitizo, kubadili maana pamoja na kuhimiza jambo. Data inaonesha kuwa katika lugha ya Kihaya, baadhi ya maneno yakiradidiwa huonesha kufanyika kwa jambo pasipo mpangilio maalumu au ukosefu wa umakini tofauti na maneno yasiyoradidiwa. Mathalani, maana ya neno *gamba* ni *ongea*. G*ambagamba* ni neno radidiwa ambalo linamaanisha tendo la kuongea hovyohovyo au pasipokuwa na umakini katika kile kinachoongelewa lakini pia kuongea bila mpangilio maalumu. Aidha, uradidi katika lugha ya Kihaya huonesha kutendeka mara kwa mara kwa tendo fulani. Yapo maneno kadhaa ambayo yakitamkwa pasipo kuradidiwa hurejelea dhana ya kufanyika mara moja kwa tendo husika au kutokuwa bayana kama tendo hilo limefanyika mara moja au mara kwa mara. Lakini pale maneno hayo yanapofanyiwa uradidi, moja kwa moja hurejelea dhana ya kufanyika mara kwa mara kwa tendo husika. Mathalani, neno la Kihaya *tonga* lenye maana ya dai, kabla ya kufanyiwa uradidi huelezea ni kwa jinsi gani mtu huweza kukumbushia kile kinachodaiwa kutoka kwa muhusika. Baada ya kufanyiwa mchakato wa uradidi neno hili hujitokeza kama *tongatonga*. Maana yake ni kuwa mtu au laweza kuwa taifa, basi mtu au taifa hilo hafanya tendo la kudai mara kwa mara au mara kadhaa. Aidha, matokeo ya makala hii yanaonesha pia kuwa moja ya dhima za uradidi katika lugha ya Kihaya ni kuonesha uharaka wa tendo husika. Imethibitika kuwa baadhi ya maneno ya Kihaya yakifanyiwa uradidi huonesha hali ya tendo kufanyika haraka zaidi kuliko neno lisilo radidiwa. Mathalani, maana ya neno la Kihaya *byala* ni panda. Pale linapofanyiwa uradidi, neno hili hujitokeza kama *byalabyala* na hurejelea tendo la kupanda harakaharaka. Dhima nyingine iliyojitokeza katika makala hii ni dhima ya kudunisha maana. Baadhi ya maneno ambayo yakitamkwa au kuandikwa pasi na kuradidiwa huimarisha maana katika lugha inayoshughulikiwa katika makala hii; lugha ya Kihaya. Pale tu maneno hayo yanaporadidiwa moja kwa moja hudunisha maana husika. Kwa mfano, neno la Kihaya *murungi* humaanisha mzuri. Dhana tunayoipata kutokana na neno murungi ni kwamba mtu fulani anakuwa na uzuri wa kiwango cha juu. Uzuri unaoongelewa hapa ni ule wa mwonekano wa nje. Neno *murungirungi* linarejelea uzuri wa kiwango cha chini au wa kawaida ikilinganishwa na neno *murungi*. Halikadhalika, imegundulika kuwa neno la Kihaya *obushuma* lenye kumaanisha wizi hukubali mchakato wa uradidi. Baada ya neno hili kuradidiwa tunapata neno *obunshumanshuma* pia laweza kuwa *orunshumanshuma*. Maana ya neno hili radidiwa ni hali ya kuwa na wiziwizi. Hivyo, neno radidiwa *obunshumashuma/ orunshumanshuma* linadunisha hali ya wizi kutoka katika kiwango kikubwa na kuwa katika kiwango kidogo kwa maana ya udokozi wa vitu vidogovidogo.

Mbali na dhima hizi, imebainika pia kuwa, uradidi hufanya kazi ya kusisitiza jambo fulani. Mathalani, kielezi *mwaha* chenye maana ya sasa hivi, kikiradidiwa na kuwa *mwahamwaha* humaanisha muda huuhuu. Maana yake kama kuna jambo inabidi lifanyike, basi lifanyike muda huo pasipo kupoteza hata dakika moja. Pia neno *kwo* humaanisha hasa, endapo neno hili litaradidiwa na kuwa *kwokwokwo* humaanisha kwelikweli ama hasahasa. Uradidi pia katika lugha ya Kihaya hubadili maana ya mwanzo. Mathalani, neno *amagezi* hurejelea akili. Baada ya neno hili kufanyiwa uradidi na kuwa *amagezigezi* maana imebadilika na kuwa hali ya udanganyifu. Aidha, neno *bashatu* hurejelea au humaanisha watatu (watu watatu). Neno radidiwa *bashatubashatu* halimaanishi watu watatu tu tena, bali humaanisha zaidi ya watu watatu, ambapo dhana inayorejelewa hapa ni hali ya kuwa katika makundi ya watu watatuwatatu. Matokeo ya makala hii yanathibitisha pia kuwa uradidi huwa na dhimay a kuhimiza jambo. Kwa mfano, neno *humula* hurejelea tendo la kumnyamazisha mwenye uchungu. Maana ya pili ya neno hili ni pumzika. Endapo neno hili litatumika bila kuradidiwa, basi neno hili halioneshi msisitizo wowote. Pale linapotumika kwa kurudiwarudiwa kama *humulahumula* huonesha msisitizo wa kumnyamazisha mhusika au kumtaka apumzike.

Kwa ujumla, makala hii ina umuhimu kwa wanaisimu na hata watafiti wa lugha mbalimbali za binadamu. Aidha, makala hii imekuwa na umuhimu wa kuonesha ni kwa jinsi gani uradidi una manufaa makubwa katika lugha zetu za Kibantu hususan lugha ya Kihaya ambapo huwa na dhima tofautitofauti kama ilivyodadavuliwa hapo juu. Makala hii imeshughulikia dhima za uradidi katika mawasiliano ya Kihaya. Dhima za uradidi katika lugha nyingine haujashughulikiwa katika makala hii. Hivyo, watafiti wengine wanaweza kulishughulikia eneo hili ili kubaini dhima za uradidi katika lugha mbalimbali. Aidha, inashauriwa kuwa ziandikwe makala zenye kuangazia ruwaza za uradidi wa kategoria mbalimbali kama vile: nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi, viwakilishi, viunganishi na viwakilishi katika lugha za Kibantu na zisizo za Kibantu.

**Marejeleo**


Ashton, E.O. (1947). *Swahili Grammar* (*Including Intonation*). London: Longmans.

Chang. L.M. (1997). "Thao Reduplication". *Papers for the Eighth International Conference on Austronesian Linguistics*. Taipei: Academia Sinica.

Crystal, D. (1986). "A Dictionary of Linguistics and Phonetics". Oxford, Basil Blackwell. *Cultures* 1992, Vol. 5, 2. Uk. 113-124.

Downing, L.J. (2003). "Bukusu Reduplication". Katika *Trends in African Linguistics* 5 uk. 73-84. Lawrenceville, NJ, Africa World Press.

Kajitani, M. (2005). "Semantic Properties of Reduplication among the World's Languages". LSO Working Papers in Linguistics 5: Proceedings of WIGI 2005, 93-106 University of Wisconsin Milwaukee.

Kapinga, M.C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam, TUKI.

Kitchin, R. na Tate, N. (2000). *Conducting Reseach into Human Geography: Theory, Methodology and Practice*. United Kingdom: Peason Education Limited.

Kothari, C.R. (2004). *Reseach Methodology*; *Methods and Techniques*, Toleo la Pili. New Delhi, New Age International Publishing Ltd.

Lodhi. A.Y. (2004). "Strategies of emphasis and intensity in Swahili". Katika *Africa & Asia: Götenbborg Working Papers on Asia and African Languages and Literatures*. Uk. 142-150.

Mdee, J. S. (1996). *Sarufi ya Kiswahili: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: DUP

McCarthy, J. na Prince, A. (1993). "Prosodic Morphology: Constraint Interaction and Satisfaction". *In Linguistics Department Faculty Publication Series*. Amherrst: University of Massachusetts.

McCarthy, J. na Prince, A. (1994a). "An Overview of Prosodic Morphology" *OTS/HIL Workshop on Prosodic Morphology*. Rutgers University.

McCarthy, J. na Prince, A. (1994b). "The Emergence of the Unmarked: Optimality in Prosodic Morphology". *Technical Report 32*, Rutgers University Center for Cognitive Science.

McCarthy, J. na Prince, A. (1995). "Faithfulness and Reduplicative Identity". *Papers on Optimality Theory*, 249-384. *GLSA,* Amherst, University of Massachusetts.

Mnenuka, A. (2010). Dhima ya Uradidi katika Mawasiliano ya Kiswahili: Uimarishaji na Udhoofishaji wa Maana. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kswahili. Juz. 73 Uk. 32-44. Dar es Salaam: TUKI.

Moravcsik, E.A (1978). "Reduplicative Construction". Katika *Universals of Human Language*. London, Boston and Henley.

Mwita, L. C. (2008). "Verbal Tone in Kuria, Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kalifornia.

Novotna, J. (2000). "Reduplication in Swahili". *Afrikanistische* Arbeitspapiere (AAP).

Odden, D. (1996). "Patterns of of Reduplication in Kikerewe." Katika *OSU Working Papers in Linguistics 48,* uk. 111-149.

Polome, E.C. (1967). *Kiswahili Language Handbook*, Washington D.C, Center for Applied Linguistics.

Rubanza, Y. I. (1996a). "Dhana ya Uradidi katika Kiswahili", katika *Jarida la Uchunguzi wa Kiswahili, Juzuu 59*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, TUKI.

Tak, J. (2007). "Three Cross Linguistics Tendencies in Reduplicated" Revisited. In *Journal of Universal of Languages*, Vol. 8. Pp. 105-122.